## BENKI YA STANBIC TANZANIA

## MAELEZO NA MASHARTI YA KADI YA MALIPO

Unathibitisha kwamba umepata fursa ya kusoma na kuelewa Masharti yaliyomo katika waraka huu. **Ibara muhimu au ibara ambazo zinaweza kupunguza wajibu wetu au kusababisha hatari kwako vitakuwa kwa maandishi mazito**. Tafadhali wasiliana nasi iwapo unahitaji tufafanue masharti yoyote ambayo yanarejewa katika Mkataba au kuhusiana na matumizi ya Kadi yako. Unaweza kutuma barua pepe kwenda tanzaniaccc@stanbic.com au unaweza kupiga simu Kituo cha Mawasiliano na Wateja **Na.0800751111.**

### 1. Tafsiri

**Mmiliki akaunti, wewe au yako** ina maana ya mtu aliyeelezwa katika Fomu ya maombi, pia anajulikana kama Mmiliki kadi.

**Mmiliki wa Ziada** ina maana ya mtu ambaye Kadi ya ziada ambayo inaungana na Kadi ya Akaunti, inatolewa kwa maombi yako.

**Sheria Zinazotumika** ina maana ya sheria,kanuni, hukumu na amri za mahakama yoyote yenye mamlaka halali, benki kuu au wakala wa serikali au mamlaka yenye nguvu ya sheria katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au mamlaka yoyote husika.

**Fomu ya Maombi** ina maana fomu ya maombi ya Kadi ya Akaunti kama ilivyojazwa na kuidhinishwa na wewe, ambapo unaridhia wajibu kwa Kadi zinazotolewa chini ya Akaunti ya Kadi.

**ATM** ina maana Mashine ya Utoaji Pesa Inayojiendesha.

**Benki, sisi, yetu** au **Benki ya Stanbic** ina maana Benki ya Stanbic ya Tanzania (yenye namba ya usajili 22443) kampuni ambayo imesajiliwa rasmi kwa madeni yenye ukomo kwa mujibu wa sheria za Tanzania na/au waandamizi wake katika wanufaika.

**Siku ya Kazi** ina maana siku yoyote ukiacha Jumamosi na Jumapili au sikukuu yoyote ya kiserikali katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. **Kadi** ina maana ya Kadi ya malipo husika,pamoja, isipokuwa maudhui yanapoonyesha vinginevyo, Kadi za ziada

nyingine ambazo tunazitoa kwa maombi yako, ambazo zote zinaunganishwa na Kadi ya Akaunti.

**Kadi ya Akaunti** ina maana ya Kadi ya Malipo iliyofunguliwa kwenye vitabu vyetu kwa jina lako kuhusiana na Mkataba huu.

**Mwenyekadi** ina maana ya mtu ambaye Kadi imetolewa kwake. Katika mkataba huu marejeo kwa Mwenyekadi inaweza kujumlisha Mwenyekadi ya Ziada au Wenyekadi za Ziada kadiri inavyoweza kuonyeshwa na muktadha wenyewe.

**Kifaa cha Kielektroni**ina maana ya kifaa cha kielektroni chochote ambacho kinatumika kukamilisha muamala na inajumlisha (bila ya ukomo) simu, ATM, maombi ya simu, tovuti au kifaa cha sehemu ya mauzo.

**Tarehe ya utekelezaji**ina maana ya tarehe ya utendaji wa Mkataba huu na mtu anayetia saini mwisho.

**Kundi** ina maana ya Kundi la Benki ya Stanbic lenye ukomo wa madeni, na tanzu zake.

**Mastercard**ina maana Mastercard Worldwide, chama cha kadi na kampuni zake husika.

**Muhimu** ina maana ya kitu chochote ambacho ni muhimu kwa mujibu wa maoni ya Benki.

**Mfanyabiashara ina maana ya msambazaji bidhaa au huduma.**

**Wahusika** ina maana wewe na sisi na Mhusika ina maana ya mmoja kati yetu kadiri maudhui yanavyoonyesha.

**Taarifa Binafsi** ina maana ya mtu anayetambulika na pale inavyostahili mtu kisheria, pamoja na taarifa kuhusu ukoo; jinsia; mimba; hali ya ndoa; utaifa; asili ya kabila au jamii; rangi; uelewa wa kijinsia; umri; afya ya mwili na akili; uwezo, ulemavu; dini ; imani; utamaduni; lugha; uzawa; elimu; tiba; kifedha; jinai au historia ya ajira; namba yoyote ya utambulisho; alama, barua pepe; anuani ya sehemu au posta; namba ya simu; eneo, utambulisho wowote kimtandao; kazi yoyote nyingine maalum kwa mtu huyo; taarifa ya kibaiometriki, maoni binafsi, mitazamo au utashi wa mtu au maoni au mitazamo ya mwingine kuhusu mtu

huyo; mawasiliano yaliyofanywa na mtu huyo ambayo kwa siri au dhahiri ni binafsi au ya siri au mawasiliano ya ziada ambayo yatabainisha maudhui ya mawasiliano ya awali, na jina la mtu huyo iwapo linaonekana na taarifa za mtu mwingine kuhusiana na mtu huyo au iwapo kufichua jina lenyewe tu kutafichua taarifa ya mtu huyo.

**PINI** ina maana ya namba ya utambulisho ya mtu inayotumika kwa matumizi ya Kadi yako.

**Kutayarisha** ina maana ya kila utendaji au kitendo, kwa mashine au la, kuhusiana na taarifa binafsi, pamoja na mabadiliko, uzuiaji, ulinganishaji daraja, uharibifu, usambazaji kwa njia ya upelekaji,usambazaji au kuwezesha kupatikana kwa njia nyingine yoyote, kufuta, kuunganisha, umoja,stakabadhi, kurekodi, urudishaji, uhifadhi, uboreshaji, ubadilishaji au utumiaji; Tayarisha na Tayarishwa itakuwa na maana moja.

**Shughuli Zilizozuiwa** ina maana ya vitendo haramu au vya kigaidi, utakatishaji pesa au vitendo ambavyo vinahusika na vizuizi au haviendani na Sheria Husika.

**Mtu Aliyezuiliwa** ina maana ya :

(a) mtu halisi au kisheria au nchi;

(b) ikiwa ni mtu kwa mujibu wa sheria,ni mtu yeyote ambaye (i) anamiliki au kuhodhi ( na kwa mujibu wa madhumuni haya, kumiliki ni kuhodhi asilimia yoyote ya umiliki au faida ya kimaslahi na kuhodhi ina maana ya uwezo, wa moja kwa moja au vinginevyo na iwe kwa kupiga kura ya hisa, uteuzi wa wakurugenzi au maafisa wa mfano wake au kupitia njia nyingine, kumiliki biashara au sera za mtu wa kisheria).

(c) ikiwa ni kwa nchi yoyote, itakuwa wizara zake,idara, wakala au shirika jingine la kiserikali, vilivyoorodheshwa katika Orodha yoyote ya Kuzuia au ambaye anawajibika na vizuizi vyovyote.

**Mamlaka ya Uwekaji Vikwazo** ina maana ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC), Ofisi ya Udhibiti wa Mali za Kigeni za Idara ya Hazina ya Marekani (OFAC), Umoja wa Ulaya (EU), Hazina ya Malkia, Wizara ya Uchumi, Fedha na Viwanda ya

Ufaransa(Ufaransa) (MINEFI) au Mamlaka yoyote ya Uwekaji Vikwazo tunayoitambua mara kwa mara.

Orodha Iliyowekewa Vikwazo ina maana ya orodha ya Taasisi Zilizowekewa vikwazona Mamlaka ya Uwekaji Vikwazo kadiriinavyorekebishwa mara kwa mara.

**Vikwazo** ina maana ya vizuizi vyovyote vilivyowekwa na Mamlaka ya Uwekaji Vikwazo,pamoja na lakini sio pekee,kidiplomasia, usafiri, biashara au vikwazo vya kifedha au vizuizi.

**Msimbo wa Usalama** ina maana ya huduma ya usalama inayotoa ithibati kwa mtandao wakati mmiliki Kadi ananunua bidhaa au huduma kutoka tovuti mbalimbali za wafanyabiashara. Ni msimbo binafsi kama PINI inayokupatia ulinzi dhidi ya matumizi yasiyoidhinishwa ya Kadi yako unapofanya ununuzi katika tovuti mbalimbali za wafanyabiashara.

**Ada ya Huduma** ina maana ada tunayoitoa kuhusiana na gharama za kawaida za utawala kwa kuhudumiaAkaunti ya Kadi.

**Muamala** ina maana ya muamala wowote wa kutoka Akaunti yako ya Kadi na inajumlisha muamala wowote uliofanya kwa Kadi, namba ya Kadi na/au PINI kulipia bidhaa au huduma zozote, kutoa pesa au kufanya muamala kwa kutumia Kifaa cha Kielektroni.

Ada za Muamala ina maana ya ada tunazoweza kutoza kwa ajili ya gharama za kimiamala ya kuendesha Akaunti ya Kadi tofauti na Ada ya Huduma.

**VISA** ina maana ya Chama cha Kimataifa cha Huduma za Visa, Chama cha kadi na kampuni zake zozote zinazohusika.

## 2. Tafsiri

2.1 Maneno yaliyotafsiriwa (kwa ajili ya uwiano) yataanza na Herufi kubwa.

2.2 Pale ambapo siku zozote zinarejewa kwenye Mkataba huu, itajumlisha Siku za Kazi tu na itaondoa siku ya mwanzo na kujumlisha siku ya mwisho.

2.3 Ikiwa tunatakiwa kutekeleza hiari yetu katika Mkataba huu, tutafanya hivyo kwa busara.

2.4 Umoja unajumlisha wingi na kinyume chake, na jinsia yoyote inajumlisha jinsia nyingine.

2.5 Vichwa vya habari vyoteni kwa ajili ya urahisi tu na havitakiwi kuzingatiwa kwa madhumuni ya kutafsiri mkataba huu.

2.6 Kila kipengele cha Mkataba huu kitazingatiwa iwe kimeainishwa kwenye sehemu ya tafsiri au kwingine katika Mkataba huu.

2.7 Sheria zote zilizotajwa katika Mkataba huu zinajumlisha sheria kuu, sheria ndogo na Kanuni zilizotajwa katika sheria hizo kuanzia tarehe ya Utumiaji na Kadiri inavyorekebishwa mara kwa mara.

**3. Uhalali wa Kadi**

3.1 Wamilikikadi sharti watie saini Kadi zao nyuma mara tuwanapozipata. Kadi isiyotiwa saini isitumike.

3.2 Mmiliki wa kadi pekee ndiye anaweza kutumia Kadi.Kadi isihawilishwe kwa mtu mwingine yeyote wala Mmiliki Kadi asiruhusu mtu mwingine kuitumia.

33. Kila Kadi ina muda wa ukomo na ni halali hadi siku ya mwisho ya tarehe na mwezi ilioonyeshwa.

**4. Utumiaji Kadi yako**

4.1 Mmilikikadi anaweza kutumia Kadi kulipia bidhaa na huduma kwa wafanyabiashara wanayoikubali Kadi hiyo. Mara Kadi inapotumika kwa Muamala kupitia kifaa cha Kielektroni, wewe au Mmilikikadi wa nyongeza hamtaweza kuondoa mamlaka hayo au kutuelekeza kusimamisha malipo yoyote ambayo tunataka kuyafanya kwa Mfanyabiashara kwa muamala wowote au kubadilisha malipo ambayo yamekwisha fanywa na sisi.

4.2 Wakati wa malipo, Mmilikikadi sharti atie saini karatasi ya Muamala iwapo Mfanyabiashara atataka. Mmilikadi hana

haja ya kutia saini karatasi ya muamala anapofanya miamala ya mbali kama kuagizia kupitia intaneti.

4.3 Kila Kadi iliyounganishwa na Akaunti ya Kadi itapewa PINI tofauti. PINI itamruhusu Mmilikikadi, pamoja na mambo mengine, kukamilisha miamala ya sehemu ya mauzo ya " kata na PINI" na kutumia nyenzo za huduma za kibenki kujisaidia kufanya Miamala kama kutoa pesa, kuweka na uhawilishaji pesa.

4.4 **Ikiwa unatumia Kadi yako kwa madhumuni ya kimtandao,** tafadhali hakikisha kwamba unachukua hatua zote muhimu kulinda usalama wako wa mtandao na faragha. Ni wajibu wa Mmilikikadi kututahadharisha mara moja kuhusu miamala yenye shaka au kutoidhinishwa katika Kadi yao.

**4.5 Tunaweza kukutoza Ada ya Muamala tofauti kwa ajili ya Miamala mingine. Orodha kamili ya ada zetu inapatikana katika matawi yetu au kwenye tovuti www.stanbicbank.co.tz**

**4.6 Wajibu wa kutulipa unaanza wakati Kadi, namba ya Kadi na/ au PINI inatumika kwa Muamala.**

4.7 Mmilikikadi sharti atimize taratibu zetu za uthibitisho kuweza au kutumia kadi zao. Sharti uhakikishe kwamba Mmilikikadi hatoi taarifa za ndani za taratibu hizi za uthibitisho na misimbo au taarifa nyingine yoyote ambayo itaonyesha utambulisho wa au taarifa za ndani za Kadi zao na mtu yeyote. Kwa mfano, Mmilikikadi asimueleze mtu yeyote namba ya utambulisho wao au namna ya kuwatambua kama wamilikikadi.

4.8 Ikiwa Mmilikikadi au mtu yeyote anatumia PINI iliyotolewa kwa Kadi, tutachukulia miamala hii kama imethibitishwa na wewe. Utawajibika kwa Miamala yote kwenye Kadi hiyo.

4.9 Ni wajibu wa Wamilikadi kuzijua na kuzitekeleza kwa ukamilifu pesa zinazotumika. Tunawajibika kutoa taarifa Benki Kuu kuhusu miamala yote inayotokea nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**4.10 Sharti uhakikishe kwamba Kadi inatumika kwa Miamala halali tu**

4.11 Hatutawajibika kwako au Mmilikikadi ikiwa Mfanyabiashara au Kifaa cha Kielektroni chochote havikubali Kadi au ikiwa tunakataa kuidhinisha Muamala wowote.

4.12 Mmilikikadi anaweza kukataa Muamala usiotumia PINI lakini sharti uthibitishe kwamba ulikuwa haukuidhinishwa kabisa. Ikiwa Mmilikikadi anataka kukataa Muamala sharti wawasiliane au kupiga simu Kituo chetu cha Mawasiliana na Mteja Na. O800751111 ndani ya siku tisini baada ya Muamala kufanyika. Tutachunguza mgogoro baada ya kupokea nyaraka muhimu kuthibitisha kwamba Mmilikikadi hakuidhinisha muamala. Hutakuwa na madai endapo hutatushauri ndani ya muda huo.

**5. Miamala ya Msimbo wa Usalama**

5.1 Miamala ya Msimbo wa Usalama ni huduma inayokupatia usalama wa ziada unapofanya ununuaji dukani kwenye intaneti kwa kutumia Kadi yako kwenye tovuti ya Mfanyabiashata iliyoandikishwa kwenye huduma ya Msimbo wa Usalama. Hata hivyo haitoi dhamana kwenye tovuti (au bidhaa au huduma zinazotolewa kwenye tovuti hizo).

5.2 Huna haja ya kujisajili kwa ajili ya huduma za Msimbo wa Usalama; Benki yenyewe imeorodhesha kadi yako kwenye huduma hiyo.

5.3 Benki inatoa huduma hii kwako,lakini tunaweza kutumia watu wengine kutoa huduma au sehemu yake kwa niaba yetu. Kwa kutumia Huduma ya Msimbo wa Usalama unaidhinisha Benki kutumia taarifa nyingine zako na Kadi yako, na watu wengine.

5.4 Benki haitawajibika kwa kushindwa kwa aina yoyote kwa Huduma za Msimbo wa Usalama unaosababishwa na matukio ambayo hatuwezi kuyazuia. Kushindwa huko kunaweza kujumlisha kutopatikana kwa nywila ya wakati mmoja iliyoombwa na wewe, au kutofanya kazi kwa nywila ya wakati mmoja kutokana na sababu yoyote. Unawajibika pekee kwa kuweka siri ya nywila yako ya wakati mmoja na kuhakikisha kwamba taarifa zako za mawasilano zinawekwa vizuri mara kwa mara kwenye mifumo yetu ili kuweza kutumia huduma hiyo inapotakiwa.

5.5 Aidha unakiri na kukubali kwamba unawajibika moja kwa moja kwa miamla yote au vitendo vingine vinavyotokea au kufanywa na Kadi yako kwa kutumia Msimbo wa Usalama wa Kadi yako.

5.6 Huduma ya Msimbo wa Usalama inaweza kurekebishwa au kukatishwa, kwa muda au moja kwa moja bila ya taarifa ya awali.

**6. Miamala kwa Mguso**

6.1 Teknolojia ya miamala bila mguso itakuwezesha kufanya malipo haraka kiurahisi na usalama kwa ununuaji wa gharama ya chini kwa kugusa tu Kadi yako kwenye kituo cha mauzo bila ya kuhitaji PINI au uthibitisho wowote kutoka kwako kama Mmilikikadi. Kwa ununuaji wa gharama kubwa utatakiwa kuingiza PINI yako kama kawaida.

6.2 Utaweza tu kufanya malipo kwa mguso kwa wafanyabiashara ambako utaona nembo ya MasterCard au VISA kukubali malipo kwa mguso.

6.3 Unapogusa Kadi yako iliyowezeshwa malipo kwa mguso unatoa ruhusa kwa Benki kutoa katika Kadi yako au bakaa ya akaunti yako kwa kiasi unachohitaji kwa ununuzi pamoja na ada inayohusika.

**7. Matumizi yasiyoidhinishwa ya Kadi yako na PINI**

7.1 Mmilikikadi sharti atuarifu mara moja anapogundua kwamba Kadi imepotea au imeibwa, au kwamba PINI imejulikana na

mtu mwingine. Tutasitisha Kadi haraka iwezekanavyo baada ya kuombwa kufanya hivyo. Kutoa taarifa ya kupotea au kuibwa kwa Kadi au PINI iliyohatarishwa tafadhali piga Kituo cha Mawasiliano na Mteja Na 0800 751111 au tutumie baruapepe kupitia tanzaniaccc@stanbic.com.

**7.2 Iwapo upoteaji au wizi wa Kadi au kuhatarishwa kwa PINI hakutatolewa taarifa haraka, utawajibika kwa Miamala yote iliyofanywa na Kadi kabla ya kuisitisha. Utawajibika kwa Muamala wowote ambapo saini ya Mmilikikadi inaonekana kwenye karatasi ya Muamala wa Kadi au kumbukumbu inayothibitisha matumizi ya Kadi au kama tuna ushahidi kuthibitisha kwamba Mmiliki kadi aliidhinisha au alihusika na matumizi ya Kadi hiyo.**

**8. Dhamana, makubalina na fidia**

8.1 Unadhamini na kutujulisha kuhusu Tarehe ya Kuanza kutumika na kwa muda wa Mkataba huu kwamba tangu maombi yako ya Kadi ya Malipo benki:

8.1.1 umekuwa na uwezo kamili kutenda na kutekeleza majukumu yako kwa masharti ya Mkataba huu;

8.1.2 masharti ya Mkataba huu hayajakinzana na au kufanya ukiukaji wa masharti ya mkataba mwingine wowote au makubaliano au kitendo kinachokulazimu;

8.1.3 nyakati zote utatekeleza Sheria zinazohusika pamoja na sheria zote dhidi ya utakatishaji fedha na ugaidi na sheria zote za mazingira na uwajibikaji;

8.1.4 pale inapohusika, umetimiza na utatimiza kanuni zote za ubadilishaji fedha na uamuzi kuhusiana na Mkataba huu mara kwa mara.

8.**2 Kadiri inavyoruhusiwa na Sheria, unatufidia kutokana na hasara zote, uharibifu, faini na/au adhabu dhidi yetu kutokana na:**

**8.2.1 utegemeaji taarifa iliyotolewa na wewe kuhusiana na Mkataba huu ; na/au**

**8.2.2 ukiukaji wa dhamana yoyote iliyowekwa na wewe chini ya Mkataba huu.**

**9. Gharama, Ada na Tozo**

Tunaweza kutoza na kufidia ada, pamoja na ada zifuatazo, iwapo zitahusika na Mkataba huu.

9.1.1 Ada ya Huduma;

9.1.2 Ada ya Muamala; na

9.2 Gharama zote, ada na tozo kuhusiana na Mkataba huu zitatolewa kwenye Akaunti ya Kadi.

**10. Uvunjwaji wa Mkataba huu**

10.1 Unaweza kuvunja Mkataba huu muda wowote kwa taarifa ya awali kwetu.

10.2 Utabaki kuwajibika kwa:

**10.2.1 malipo yoyote yaliyobaki na ununuaji baada ya uvunjwaji. Kuna nyakati ambapo Miamala bado inaweza kufanywa hata baada ya kufungwa kwa Akaunti ya Kadi . Hii inajumlisha maelekezo ya malipo ya madeni yaliyopo na malipo dhidi ya Akaunti ya Kadi ambayo hayajafutwa na wewe na/au Wamilikikadi wa Nyongeza. Pia inajumlisha miamala ya Kadi ambayo inafanywa nje ya mtandao baada ya Akaunti ya Kadi kufungwa. Utawajibika na utahusika na Miamala yote hiyo hata baada ya kufungwa kwa Akaunti ya Kadi;**

10.2.2 majukumu yoyote kutokana na Mkataba huu iwapo unashindwa kutuarifu kwamba Akaunti ya Kadi imefungwa;

10.2.3 **Mara baada ya Akaunti ya Kadi kufungwa, sharti uhakikishe kwamba** Mmilikikadi yeyote wa Nyongeza

ambaye amepewa maelezo ya Kadi ameshauriwa kwamba hawataweza tena kuitumia. Pia sharti uhakikishe kwamba Kadi au kadi zote zinateketezwa mara moja kwa kukata katikati ya mstari wa sumaku, kibanzi na namba ya akaunti na kukwangua namba zinazoonekana sehemu ya kuweka saini katika Kadi. **Kadi ambayo haikuharibiwa vizuri bado inaweza kutumika.Ikitokea hivi utawajibika kwa Miamala hii.**

10.4 Siku zote Kadi itakuwa mali yetu bila ya kupoteza haki ya madai yoyote dhidi yako ikiwa:

10.4.1 kwa jumla unafanya au kuacha kufanya chochote ambacho kinaweza kufanya tupate hasara au uharibifu;

10.4.1.2 wewe unakuwa au unaweza kuzuiwa au tunajua au kushuku kwamba Akaunti yako ya Kadi inatumika kiudanganyifu, kizembe, kiuhalifu au vitendo vya kigaidi, au kwa kitendo chochote ambacho hakifuati Sheria zinazohusika au ikiwa unahusika katika vitendo vyovyote haramu au vya kigaidi.

10.**5 Ikiwa tutafunga, kuzuia au kusitisha matumizi ya Kadi yako kwa sababu yoyote ile, hatutawajibika kisheria moja kwa moja au vinginevyo kwa hasara yoyote inayotokana na kitendo hicho ambayo wewe au mtu mwingine anaweza kupata mpaka hasara hizo ziwe zinatokana na uzembe wetu mkubwa au wakala wetu au mtu yeyote anayedhibitiwa na sisi.**

**11. Makatao ya Madai**

**11.1 Benki haitawajibika kwa kushindwa kutekeleza majukumu yoyote humu yanayotokana na sababu nje ya uwezo wetu moja kwa moja au vinginevyo kutokana na kutenda au kutokutenda kwa serikali, fujo, migomo, mapinduzi, vizuizi, uasi wa kiraia, kadari ya Mungu, mabadiliko katika sheria au mabadiliko makubwa katika hali ya soko. Inapotakiwa Benki itakujulisha mapema kupitia njia mbalimbali, pamoja na ujumbe mfupi, barua pepe, barua au taarifa kwenye ATM,**

**kwenye matawi yetu na njia nyingine ambazo zitakuwa lazima kutumika kwa nyakati tofauti.**

**11.2 Unakubali kuwa (i) Vifaa vya Kielektroni haviko chini ya uwezo wetu; na (ii) huduma zetu zinaweza kukosekana kutokana na muingiliano wake na matengenezo ya mtandao wetu wa mawasiliano ya kielektroni au kutokana na upungufu wa umeme, mawasiliano au mazingira mengine ambayo hayako chini ya uwezo wetu. Iwapo itawezekana kwetu, tutajaribu kukupa taarifa endapo matengenezo yaliyopangwa yataingilia au kuchelewesha huduma zinazotolewa kwako.**

11.3 **Isipokuwa kwa kiwango ambacho tumefanya uzembe mkubwa au nia ya udanganyifu, hatutawajibika kwa hasara yoyote inayotokana na matumizi au kushindwa kwa Kifaa cha Kielektroni, au kutokana na kuharibika kwa mitandao saidizi au tunayochangia au kutokana na mazingira nje ya uwezo wetu wa kawaida. Hatuweki dhamana ya usalama wa Huduma ya Ujumbe Mfupi (sms) au mawasiliano mengine ambayo tunawezakuyatuma kwako kuhusiana na Akaunti ya Kadi yako.**

**11.4 Wahusika hawatawajibika miongoni mwao kwa hasara au uharibifu unaotokea. Hususan hatutawajibika iwapo utapata hasara au uharibifu endapo tutakubali au kukataa muamala unaotokana na udanganyifu na vigezo vya kasimwelekeo ambavyo tunavyo kwa ajili yako.**

**12. Anuani kwa taarifa**

12.1 Unaamua kama anuani yako kwa taarifa za kisheria kwa mujibu wa Mkataba huu, anuani kama ilivyoonyeshwa katika Fomu yako ya Maombi.

12.2 Taarifa nyingine yoyoteau mawasiliano yanayotakiwa au kuruhusiwa kutolewa kuhusiana na vipengele vya Mkataba huu vitatumika kuanzia tu iwapo vitakuwa kwa maandishi na kupelekwa kwa anuani ya taarifa, anuani ya barua pepe au ya posta uliyoitoa katika maombi yako, au anuani yoyote iliyotolewa kwa mujibu wa ibara ya 12.3 hapa chini, alimuradi

nyaraka ambazo zitatumwa kuhusiana na mienendo ya kisheria kuhusu Mkataba huu inaweza kutumwa tu kwa anuani yako ya taarifa.

12.3 Sharti utupe taarifa ya maandishi kubadilisha anuani yako, anuani ya posta, namba ya fax au anuani ya barua pepe. Mabadiliko yatanza kutumika tarehe 10 ya Siku ya Kazi baada ya kupokea taarifa yako.

12.4 Taarifa yoyote itachukuliwa kuwa imepokelewa siku ya tanoya Siku ya Kazi baada ya kutuma iwapo imetumwa kwa kusajiliwa posta, mnamo siku ya saba ya Siku za Kazi baada ya kutumwa kwa njia ya kawaida ya posta, siku ya kuwasilishwa iwapo itakuwa imetumwa kwa mkono, au siku ya kwanza ya Siku za Kazi baada ya siku ambayo imetumwa iwapo imetumwa kwa telefaksi au barua pepe.

12.5 Pamoja na mambo yote yaliyoainishwa katika ibara hii ya 12, taarifa ya maandishi au mawasiliano yaliyopokelewa na wewe itakuwa ni taarifa ya maandishi ya kutosha au mawasiliano kwako hata kama haikutumwa au kuwasilishwakwa anuani yako ya taarifa, anuani ya posta, namba ya fax au anuani ya barua pepe. Unaridhia hapa kwamba pale ambapo ofisi ya posta haitoi huduma za kupeleka za mtaa katika anuani yako ya taarifa, tunawezakutunza taarifa zozote kwa mujibu wa Mkataba huukwenye anuani yako ya posta.

12.6 Utume kwetu taarifa yako yoyote ya kisheria kwenda anuani yetu(anuani yetu ya taarifa):

Benki ya Stanbic
Kituo cha Stanbic kona
Kona ya Barabara ya Ali Hassan Mwinyi/ Konondoni
SLP 72647
Dar es Salaam
Kwa uangalifu wa Mkuu, Sheria

**13 Hawilisho la Benki**

**13.1 Kadiri inavyoruhusiwa na sheria, unaridhia kwamba tunaweza, bila taarifa ya ziada kwako, kuhawilisha na kuhamisha haki zetu zote au baadhi yake na/au kuwakilisha majukumu yote au sehemu yake chini ya Mkatba huu, ama yote au sehemu kwa mtu yeyote ingawa hawilisho hilo na/au uwakilishi unaweza kusababisha kugawanyika kwa madai dhidi yako.**

**13.2 Unaridhia kwamba hutahawilisha au kuhamisha haki zako zote au sehemuyake au kuwakilisha majukumu yako au sehemu yake chini ya Mkatataba huu mpaka uwe umepata kwanza ridhaa yetu ya maandishi.**

**14 Jumla**

14.1 Inapobidi tutakutumia mabadiliko kila mara kuhusu hadhi ya Kadi yako kwa sms kwenye namba yako ya simu iliyotolewa kwenye Fomu ya Maombi au kama tutakavyo fahamishwa baadaye kwa maandishi.

14.2 Tutakushauri kuhusu faida zozote za nyongeza **(faida)** ambazo unaweza kupata au kustahiki mara kwa mara kama Mmilikikadi. Faida hizikwa kawaida zitatumika pale Kadi inapotolewa na itatumika kwa mujibu wa maelezo na masharti ambayosharti uyatekeleze. Hatuhakikishi kwamba faida itapatikana siku zote au kwamba zitakuhusu wewe. Ikiwa utahitaji taarifa zaidi kuhusu Faida, tafadhali wasiliana na benki yako au tembelea tawi lako la karibu.

14.3 Mkataba huu unafanya mkataba wote baina ya wahusika. Iwapo ibara zozote(au sehemu yoyote ya ibara) katika Mkataba huu inaonekana kuwa havifai, haramu au havitekelezeki, hii haitaathiri ibara zilizobaki kwenye Mkataba huu ambazo zitaendelea kwa nguvu na utekelezaji wote.

**14.4 Isipokuwa pale ilipoelezwa wazi katika Mkataba huu mabadiliko yoyote muhimu kwenye Mkataba huu yataelezwa kwako mara kwa mara, kupitia sms, barua pepe au kupitia tovuti yetu kwa kukupatia taarifa ya siku thelathini (30) kabla. Isipokuwa inapoelezwa na kukubalika mahususi kwa maandishi, hakuna marekebisho kwenye Mkataba huu ambayo yatafanya mkataba mpya.Hutaruhusiwa kurekebisha Mkataba huu bila idhini yetu ya maandishi.**

**14.5 Unaridhia kwamba hatutawajibika kupata ridhaa yako ya maandishi kwa marekebisho hayo, lakini ikiwa huafikiani na mabadilisho yetu una haki ya kukatisha Mkataba huu. Unaridhia kwamba iwapo utaamua kutokatisha Mkataba huu kabla ya mabadiliko hayajaanza kutumika, yatakubana. Kuendelea kwa mtumiaji wa Kadi na Mmilikikadi na/au Akaunti ya Kadi kutachukuliwa kama kuridhia mabadiliko yoyote kwenye Mkataba.**

14.6 Kwa kadiri unavyotumia Kadi kufanya miamala kupitia mitandao yetu mingine, mathalani huduma ya Benki kwa intaneti, kanuni za mtandao huo zinatumika pamoja na Masharti haya.

14.7 Mkataba huu utasimamiwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. Unaridhia kwamba tunaweza kukushtaki katika mahakama yenye mamlaka kurejesha kiwango chochote tunachokudai katika tarehe ambayo tumefungua madai, ambayo yatajumlisha riba,tozo, ada za kisheria na gharama.

14.8 Tunawajibika kisheria kila mara kukujulisha habari zako kama vile anuani yako ya makazi, anuani ya posta na maelezo ya mawasiliano (pamoja na anuani ya barua pepe na namba ya simu). Tunaweza kuwasiliana na wewe kuhusiana na suala hili mara kwa mara.

14.9 Hakuna hisani/malipo yoyote tunayokupa yanaweza kuondoa haki zetu zozote chini ya Mkataba huu au kwa namna yoyote kuathiri haki yetu yoyote dhidi yako.

14.10 Kwa kiwango ambacho Mkataba huu au sehemu yake yoyote unaendeshwa na au kuwajibika na sheria husika, hakuna kipengele chake chochote kinakusudiwa kukiuka Sheria Husika. Vipengele vyote vya Mkataba vitachukuliwa kutosheleza kwa kiwango kinachotakiwa kuhakikisha kutekeleza Sheria husika na Mkataba huu sharti utafsiriwe na kutumika kama hivyo.

## 15 Vikwazo

15.1 Wewe na Mmilikikadi wa nyongeza asifanye yafuatayo:

15.1 kutumia Akaunti ya Kadi kugharamia mtu yeyote aliyewekewa Vikwazo;

15.1.2 kutumia mapato ya Akaunti ya Kadi kwa mtu ambaye anaweza au kukusudia kugharamia shughuli za Chombo Kilichowekewa Vikwazo;

15.1.3 kutenda kwa namna ambayo kunanufaisha Chombo Kilichowekewa Vikwazo;

15.1.4 kuhusika na vitendo vyovyote vilivyokatazwa; au

15.1.5 kutumia bidhaa au huduma yoyote inayotolewa na Kundi kwa ajili ya Vitendo Vilivyokatazwa.

15.2 Unaahidi kwamba Mmilikikadi wa Ziada yeyote sio:

15.2.1 Mtu Aliyewekewa Vikwazo; au

15.2.2 anachunguzwa kwa vitendo vyovyote kuhusiana na Vikwazo.

15.3 Sharti utufahamishe haraka kwa maandishi iwapo Mmilikikadi anachunguzwa kwa vitendo vyovyote kuhusiana na Vikwazo.

15.4 Unatufidia dhidi ya (unawajibika kwa) faini, adhabu, hasara, uharibifu, gharama, vitendo, mienendo na madai (hasara) tunavyoweza kupata kwa sababu:

15.4.1 fedha zozote zinakamatwa au kuzuiliwa na Mamlaka ya Uwekaji Vikwazo yoyote au mtu mwingine ( pamoja na sisi); au

15.4.2 Mmilikikadi anakiuka ibara hii ya 15.

15.5 Ikiwa tunajua au kushuku kwamba Mmilikikadi anakiuka ibara ya 13 au anakaribia kuwekewa Vikwazo, tunaweza mara moja, kwa hiari yetu:

15.5.1 kufunga, kataza shughuli au kuzuia matumizi ya Akunti ya Kadi na bidhaa au huduma nyingine tunazokupa; na/au

15.5.2 kukatisha Masharti haya na/au uhusiano mwingine tunaoweza kuwa na wewe.

15.6 Hatuwajibiki kwako kwa Hasara zozote unazopata endapo tutavunja Masharti haya au uhusiano mwingine na wewe.

**16. Ulinzi wa data**

16.1 Unatupa ridhaa kukusanya Taarifa yako Binafsi kutoka kwako na, iwapo ni halali na inafaa, kutoka vyanzo vya umma kuhusu mikopo, udanganyifu na madhumuni yaliyoanishwa hapa chini.

16.2 Unathibitisha kwamba, iwapo utatupa Taarifa Binafsi kuhusu au kwa niaba ya watu wengine (pamoja na wenye saini katika akaunti,wenyehisa, maafisa watendaji wakuu, wadhamini na wanufaishwa) unaruhusiwa(a) kutupatia Taarifa zao Binafsi; (b) Kuridhia kwa niaba yao kwa Taarifa Binafsi; na hususan upelekaji wa taarifa nje ya mipaka kuhusu Taarifa Binafsi kwa na kutoka nchi ambako bidhaa na huduma vinatolewa; na(c) kupokea taarifa binafsi zozote kwa niaba yao.

16.3 Unatupa ridhaa ya kutumia Taarifa yako Binafsi:

16.3.1 kwa ajili ya kukupatia bidhaa na huduma kwa mujibu wa Mkataba huu na kukupatia bidhaa nyingine na huduma unazoweza kuomba;

16.3.2 kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa kitakwimu na mwingine ili tuweze kutambua masoko muhimu na mwendo wake na kutathmini na kuboresha biashara yetu (hii inajumlisha kuboresha na kuendeleza bidhaa na biashara mpya);

16.3.3 kwenye nchi nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambako bidhaa na huduma zinatolewa. Nchi hizi zinaweza zisiwe na Sheria sawa za ulinzi wa data kama nchi ambayo bidhaa na huduma zinatolewa. Tunapoweza,tutamuomba mhusika anayepokea kuafiki sera zetu binafsi;

16.3.4 kwa kutumia pamoja Taarifa yako Binafsi na watoaji wetu huduma wengine, ndani na nje ya nchi ambako bidhaa na huduma zinatolewa. Tunaomba watu wanaotoa huduma kwetu kukubali sera zetu binafsi iwapo wanahitaji kutumia Taarifa Binafsi yoyote kufanya shughuli zao.

16.3.5 Ndani ya Kundi

16.4 Utaona Taratibu zetu za utendaji katika maelezo yetu binafsi na Kundi.Maelezo haya yanapatikana katika tovuti ya Kundi au kwa kuombwa.

16.5 Endapo huna hakika na hali yako ya kodi au kisheria kwa kuwa Taarifa Binafsi zako zinashughulikiwa katika nchi ambayo huishi au kufanya shughuli zako, pata ushauri huria.

**16.6 Utafutaji Masoko**

16.6.1 Hapa unaridhia Benki kuchangia data yako na taarifa binafsi ndani ya Kundi ikiwa lazima kwa madhumuni ya utafutaji masoko na kutoa huduma kwako.

16.6.2 Tunaweza kutumia Taarifa yako Binafsi kukueleza kuhusu bidhaa, huduma na ofa maalum kutoka kwetu au kampuni nyingine ambazo zinaweza kukuvutia. Tutafanya hivi kupitia barua pepe, ujumbe mfupi (sms), majukwaa ya kijamii au kukuarifu kwenye maombi yako ya mtandao. Ikiwa baadaye unaamua kwamba hutaki tufanye hivi, tafadhali wasiliana nasi kupitia mtandao wa huduma kwa mteja kusitisha huduma hii.

Kwa kutia saini hapa chini unaridhia kwamba Mkataba huu umeelezwa kikamilifu kwako na kwamba unaelewa haki na wajibu wako na hatari za Akaunti ya Kadi na kuridhia kwamba Mkataba huu unakubana.

Umetiwa saini________________________kwenye(YYYY-MM-DD)

| **Wamiliki akaunti** | **Namba ya Utambulisho** |
| --- | --- |
| Jina Kamili | |
| 1. _________________ | 1. _____________________ |
| 2. _________________ | 2.______________________ |

Saini za Wamiliki akaunti

| | |
| --- | --- |
| 1. _______________________ | 1. ________________________ |
| 2. ________________________ | 2. ________________________ |

**MashahidiNamba ya Utambulisho**

| | |
| --- | --- |
| Jina Kamili | |
| 1. _____________________ | 1. ____________________ |
| 2. ____________________ | 2. ____________________ |
| Saini za Mashahidi | |
| 1. _____________________ | 1. ____________________ |
| 2. ____________________ | 2. ____________________ |